**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMAII, JINSIA WAZEE NA WATOTO**

# MWONGOZO WA WAKUFUNZI WA WAHUDUMU WA AFYA KATIKA JAMII

# HUDUMA ZA UCHUNGUZI WA SARATANI ZA VIA VYA UZAZI

## Draft Desemba, 2017

# WAJIBU NA MAJUKUMU YA MHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII

## UTANGULIZI

Wajibu wa Mhudumu wa afya ngazi ya jamii ni kueleimisha na kuhamsisha jamii kufanya uchunguzi wa awali ya saratani ya mlango wa kizazi na utoaji wa rufaa kwa magonjwa ya saratani. Mhudumu wa Afya ngazi ya Jamii anawajibika kufanya shughuli ambazo zitazochochea mabadiliko ya tabia na kubuni mazingira rafiki yatakayosaidia jamii kutumia huduma za afya na kubadili tabia dhidi ya mila potofu.

Mhudumu wa Afya ngazi ya Jamii anatakiwa kutembelea angalau kaya kumi (10) katika muda wa siku kwa juma. Kwa kufanya hivyo inakadiriwa mhudumu atatembelea kaya zipatazo mia moja kwa kipindi cha robo mwaka. Aidha, atatoa elimu ya afya kwa mkusanyiko wa jamii angalau mara moja kwa juma.

Mwongozo huu unatoa muhtasari wa majukumu na wajibu maalumu ambayo Mhudumu wa Afya katika Jamii anatazamiwa kuyatimiza katika utoaji wa huduma za uchunguzi wa saratani ya via vya uzazi. Mwongozo huu unaelimisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutoa elimu ya uchunguzi wa saratani ya via vya uzazi.

**Majukumu hayo ni:**

1. Kuandaa mpango kazi.
2. Kutembelea kaya, kutoa elimu ikiwemo ya kuhimiza jamii kufanya uchunguzi wa saratani ya via vya uzazi ikiwemo: saratani ya mlango wa kizazi,saratani ya matiti na tezi dume
3. Kufanya uhamasishaji kuhusu kufanyiwa uchunguzi wa mabadiliko ya awali mapema
4. Kutoa rufaa kwa wateja kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu kwa ajili ya huduma hizi
5. Kushiriki katika mikutano ya afya ya kijiji na kushiriki katika kampeni za kitaifa.

**Mambo muhimu ya kukumbuka kwa muelimishaji wakati wa kutoa mada:**

- Jitambulishe _toa utangulizi wa somo/mada
- Zungumza malengo ya semina/mkutano/mada
- Uliza maswali kwenye kikundi
- Uliza maswali kwa mtu mmoja mmoja
- Uliza maswali tofauti tofauti (marahisi, yakiasi, magumu)
- Tumia majina ya washiriki : wakati unauliza maswali
- Toa mrejesho nyuma-chanya.
- Jibu maswali ya washirikivizuri
- Tumia maandishi maalumu au mtaala uliohakikiwa
- Macho yako yaangalie washiriki wakati wote
- Toa sauti ya kutosha_isikike vizuri kwa washiriki wote
- Zunguka kwenye chumba vizuri wakati wa kutoamada
- Tumia vifaa vya kusaidia kuona na kusikia ipasavyo
- Onyesha heshima kwa washiriki
- Toa muhtasari mzuri wa mada
- Toa nafasi kwa washiriki kujadili mada

## Utangulizi

Somo hili linawawezesha Wahudumu wa Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga na Mtoto chini ya Miaka mitano kuielewa dhana ya saratani za via vya uzazi, katika jamii ya Tanzania. Linawawezesha pia kuelewa majukumu yao muhimu katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kupunguza uwezekano wa kupata Saratani za mlango wa kizazi, matiti na tezi dume.

Wahudumu wa afya katika jamii wanao wajibu wa kutambua sababu zinazochangia kupata saratani za via vya uzazi, dalili na njia za kujingika na Saratani hizi. Jamii pia ina wajibu wa kuwasaidia wagonjwa wanaogunduliwa na Saratani ya mlango wa kizazi,matiti na tezi dume.

Somo hili linalenga kuwaongezea wahudumu wa afya katika jamii,elimu na ujuzi katika kuwasaidia jamii kuongeza uelewa juu ya saratani za via vya uzazi pamoja na dalili za saratani hizi ili kuhamasisha jamii kujenga tabia ya kufanya uchunguzi wa saratani mapema na kupewa tiba wakati muafaka.

**Muda:dakika 240**

**Malengo:**

Baada ya somo hili, mshiriki aweze:

1. Kueleza dhana ya Saratani za via vya **uzazi**
2. Kueleza kwa muhtasari sababu zinazochangia kupata saratani ya mlango wa kizazi, tabia hatarishi, dalili za ugonjwa na jinsi ya kujikinga
3. Kueleza sababu zinazochangia kupata saratani ya matiti, dalili za ugonjwa na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata saratani hii
4. Kuelimisha jamii sababu zinazochangia kupata saratani ya tezi dume, dalili za ugonjwa na njia za kupunguza uwezekano wa kupata Saratani hii
5. Kutoa unasihi kwa wateja kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi mapema kuzuia saratani za via vya uzazi na kuonyesha kwa vitendo namna ya kujichuguza Saratani ya matiti
6. Majukumu na wajibu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo an Saratani za via vya uzazi
7. Kutambua wateja wanaotakiwa kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa saratani za via vya uzazi
8. Kutoa ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi
9. Kuainisha imani na fikra potofu ndani ya jamii kuhusu saratani za via vya uzazi

**MUHTASARI WA SOMO:**

| Na. ya Lengo | Lengo | Muda |
|---|---|---|
| -- | Utangulizi | **Dakika 5** |
| **1.** | Dhana ya Saratani za via vya uzazi | **Dakika 5** |
| **2.** | Saratani ya mlango wa kizazi; chanzo,tabia hatarishi,dailli na jinsi ya kujikinga | **Dakika 45** |
| **3.** | Saratani ya matiti; visababishi,dalili na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata Saratani hii | **Dakika 40** |
| **4.** | Saratani ya tezi dume ; visababishi,dalili na njia za kuepuka kupata Saratani hii | **Dakika 30** |
| **5.** | Majukumu na wajibu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo an Saratani za via vya uzazi | **Dakika 30** |
| **6.** | Wateja wanaotakiwa kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa saratani za via vya uzazi | **Dakika 15** |
| **7.** | Ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi (IGIZO) | **Dakika 30** |
| **8.** | Kuainisha imani na fikra potofu ndani ya jamii kuhusu Saratani za via vya uzazi | **Dakika 15** |
| **9.** | Tathmini na maswali | **Dakika 25** |
| **JUMLA** | | **Dakika 240** |

**9.0 UTANGULIZI**

**Muda**: Dakika 5
**Njia za kuwezesha:** Majadiliano ya mvuno; wawili wawili na majadiliano ya wote
**Nyenzo/Vifaa:karatasi kubwa /projekta ya kielektroniki**

**Maelekezo kwa mwezeshaji:**

**HATUA YA KWANZA:**

Wasalimu washiriki na uwakaribishe kwenye somo

**HATUA YA PILI:**

- Bandika karatasi kubwa iliyoandikwa malengo ya somo
- Mwambie mshiriki mmoja asome malengo ya somo kwa sauti
- Waulize washiriki kama wana maswali yoyote kuhusiana na malengo husika

**HATUA YA TATU:**

- Waulize washiriki wanaelewa nini kuhusu Saratani za via vya uzazi na kama wameshamwona mgonjwa mwenye saratani. Wape washiriki nafasi wajadili wawili wawili kuhusu huduma za Saratani za via vya uzazi ambazo wanazitoa katika jamii zao na kuuliza ni nani hasa anayezitoa.

**HATUA YA NNE:**

- Jadili majibu yatakayotolewa na washiriki baada ya bunga bongo. Hitimisha kwa kuwaambia washiriki kwamba lengo la somo ni kuimarisha elimu yao katika uhamasishaji wa umuhimu wa kufanya uchunguzi mara kwa mara wa Saratani za via vya uzazi ili kupunguza vifo vitokanavyo na saratani hizi. Taja aina za saratani za via vya uzazi zilizolengwa kwenye mada hii.

**9.1 Dhana ya Saratani za via vya uzazi**
**Muda:** Dakika 5
**Njia za kuwezesha:** **Majadiliano ya wote**
**Vifaa:** Chati pindu/projekta ya elektroniki

**Maelekezo ya mwezeshaji**
**Hatua ya Kwanza**: Waulize washiriki Saratani/kansa ni nini? Inaelewake kwenye jamii ?
**Hatua ya Pili:** Ongeza au sahihisha maelezo yao kwa kuwapa taarifa sahihi.
**Hatua ya Tatu:** Tumia slides kuwasilisha mada na waelimishe maana ya saratani na saratani za via vya uzazi
**Hatua ya Nne:** Hitimisha kwa kuboresha uelewa wa Saratani na mpango wa kitaifa wa kuzuia Saratani za via vya uzazi

**HATUA YA KWANZA:**

Waulize washiriki, je mnafahamu Saratani/kansa ni nini? Toa nafasi kwa washiriki wachache kujaribu kujibu swali hili ili uweze kupima uelewa wao

**HATUA YA PILI:**

**Eleza mambo muhimu yafuatayo:** Saratani ni nini, Saratani za via vya uzazi ni zipi na tofauti ya Saratani hizi. Onyesha mchoro ili kuboresha uelewa wao kwenye viungo vya uzazi.

**HATUA YA TATU:**

Wasilisha mada na ruhusu maswali kuongeza uelewa.

**HATUA YA NNE:**
Waambie washiriki warudie walichojifunza kwa ufupi. Boresha uelewa wao kwa kuzingatia yafuatayo;

- Saratani ni nini
- Saratani za via vya uzazi ni zipi
- Programu ya kitaifa ya kuzuia Saratani za via vya uzazi

**9.2 Muhtasari wa Saratani ya mlango wa kizazi (chanzo/visababishi,dalili na jinsi ya kujikinga)**
**Muda:** Dakika 45
**Njia za uwezeshaji:** Majadiliano ya wote, kuwasilisha mada kwa kutumia slides
**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki

**Maelekezo kwa mwezeshaji:**
**Hatua ya Kwanza:** Wasilisha kwa kifupi na tumia takwimu muhimu kuhusu saratani ya mlango wa kizazi
**Hatua ya Pili:** Ongoza majadiliano kuhusu chanzo za Saratani ya mlango wa kizazi.
**Hatua ya Tatu:** Ongeza au punguza maelezo kadiri inavyohitajika, tumia slides kuwasilisha mada inayohusu Saratani ya mlango wa kizazi
**Hatua ya Nne:** Hitimisha kwa kuboresha uelewa wa Saratani ya mlango wa kizazi na njia mbali mbali zinazoweza kutumika kupunguza uwezekano wa kupata Saratani hii.Waelimishe wapi wanaweza kupata huduma za uchunguzi wa Saratani hii katika Mkoa husika

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waulize washiriki iwapo wanaelewa ni wanawake wangapi hapa Tanzania wanapata Saratani ya mlango wa kizazi. Ni wanawake wangapi wanakadiriwa kupoteza maisha katika jamii ya Tanzania. Waulize ni asilimia ngapi ya wanawake wanopata saratani wanapoteza maisha.

- Waeleze washiriki kuwa hapa Tanzania,kulingana na takwimu za Hospitali ya Saratani ya Ocean Road,Saratani ya mlango wa kizazi inachangia kwa kiasi kikubwa kupoteza maisha ya wanawake wa Tanzania. Kwa takriban zaidi ya miaka10 iliyopita Saratani hii imekua ikiongoza kuathiri kina mama zetu. Asilima 40 ya wagonjwa wote wa saratani wanotibiwa katika Hospitali hii ni wanawake wenye Saratani ya mlango wa kizazi. Katika mwaka 2014/2015, Taasisi ya Saratani Ocean Road, ambayo ni Taasisi pekee inayotoa matibabu ya saratani, ilihudumia wagonjwa wapya 5,681 wakiwemo wagonjwa wapya wa saratani ya matiti 733 na wagonjwa wapya 1,867 wa saratani ya mlango wa kizazi. Wagonjwa hawa wanaoweza kufika Ocean Road ni asilimia 10 tu ya wagonjwa wote wa saratani wanaokadiriwa kuwepo nchini.

- Inakisiwa kwa kila wanawake 100,000, 54 walikadiriwa kupata ugonjwa huu kwa Mwaka 2012 kulingana na takwimu za ripoti ya Globocan na kati yao takriban 32.4 walipoteza maisha. Tanzania ni kati ya nchi zinazoongoza kwa vifo vya wanawake kutokana na Saratani hii katika bara la Africa.

- Takwimu za ulimwengu zinaonyesha takriban wanawake 528,000 walipata Saratani ya mlango wa kizazi Mwaka 2012 na kati yao asilima 50 walipoteza maisha (wanawake 266,000).

**HATUA YA PILI:**

- Ongoza majadiliano kuhusu chanzo za Saratani ya mlango wa kizazi
- Waambie washiriki wajadili kuhusu sababu zinazosababisha Saratani ya mlango wa kizazi.

- Wape dakika 3 kujadili
- Angalia slides kuhakiki uelewa wao na kuelimisha

**HATUA YA TATU:**

- Tumia slides kuwasilisha mada inayohusu Saratani ya mlango wa kizazi
- Karibisha maswali ili kuboreha uelewa wao
- Hakikisha yafuatayo yanatajwa kuhusu dhana inayohusu Saratani ya mlango wa kizazi;
    - Tabia hatarishi zinazochangia kusababisha Saratani ya mlango wa kizazi
    - Dalili za Saratani ya mlango wa kizazi
    - Jinsi ya kujikinga na Saratani ya mlango wa kizazi
    - Faida ya kufanya uchunguzi wa mabadiliko ya awali mapema
    - Walengwa wa uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi
    - Wajibu wa watoa huduma ngazi ya jamii kuhamasisha uchunguzi na tiba ya mabadiliko ya awali ya Saratani ya mlango wa kizazi
    - Vituo vinavyotoa huduma za uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi kaika eneo husika

**HATUA YA NNE:**

- Hitimisha kwa kuboresha uelewa wa Saratani ya mlango wa kizazi na mpango wa kitaifa wa kuzuia Saratani hii
- Jukumu la watoa huduma ya afya kusaidia huduma ya uchunguzi na tiba ya Saratani ya mlango wa kizazi
- Mwezeshaji atoe muhtasari wa masuala muhimu katika somo na kuulia maswali kwa washiriki

**9.3 Muhtasari wa Saratani ya matiti (**visababishi, dalili na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata Saratani hii)

**Muda:** Dakika 40

**Njia za uwezeshaji:** Majadiliano ya wote, kuwasilisha mada kwa kutumia slides

**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki

**Maelekezo kwa mwezeshaji:**

**Hatua ya Kwanza:** Toa muhtasari wa Saratani ya matiti Tanzania. Wasilisha kwa kifupi takwimu muhimu kuhusu saratani ya matiti kuelimisha washiriki ukubwa wa tatizo

**Hatua ya Pili:** Ongoza majadiliano kuhusu vichocheo vinavyovyosababisha Saratani ya matiti

**Hatua ya Tatu:** Elimisha washiriki kuhusu dalili na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata Saratani ya matiti na walengwa kwenye uchunguzi huu

**Hatua ya Nne:** Fafanua inavyowezekana, karibisha maswali na fanya majumuisho

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waulize washiriki wamesikia nini kuhusu saratani ya matiti.Je wanaume wanaweza kupata saratanai ya matiti?

- Waeleze washiriki kuwa hapa Tanzania, kulingana na takwimu za Hospitali ya Saratani ya Ocean Road, Saratani ya matiti inawaathiri wanawake wengi kuliko wanaume.

Inakadiriwa kati ya wagonjwa 100 wenye Saratani ya matiti, mmoja atakuwa mwanaume (10%).Wengi hufika kwenye Hospitali hii wakiwa katika hatua za mwisho za ugonjwa.

- Takwimu za ulimwengu zinaonyesha takriban asilimia 14.4% waligunduliwa na Saratani ya matiti Mwaka 2012 Tanzania (Globocan).

**HATUA YA PILI:**

- Ongoza majadiliano kuhusu vichocheo vinavyosababisha Saratani ya matiti.
- Wagawe washiriki katika makundi na wajadili vichocheo vinavyosababisha Saratani ya matiti kwa dakika 5
- Waambie washiriki wawasilishe maoni yao
- Tumia slides kuelimisha na kuboresha uelewa wao na fanunua vichocheo mbalimbali vinavyochangia kusababisha Saratani ya matiti

**HATUA YA TATU:**

- Tumia slides kuelimisha washiriki kuhusu dalili na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata Saratani ya matiti na walengwa kwenye uchunguzi huu
- Karibisha maswali ili kuboresha uelewa wao
- Hakikisha yafuatayo yanatajwa kuhusu dhana inayohusu Saratani ya matiti;
    - Vichocheo, sababu zinazochangia kupata Saratani ya matiti
    - Dalili za Saratani ya matiti
    - Jinsi ya kuzuia uwezekano wa kupata Saratani ya matiti
    - Faida ya kufanya uchunguzi wa Saratani ya matiti
    - Walengwa wa uchunguzi wa Saratani ya matiti
    - Wajibu wa watoa huduma ngazi ya jamii kuhamasisha uchunguzi wa Saratani ya matiti
    - Vituo vinavyotoa huduma za uchunguzi wa Saratani ya matiti katika maeneo husika

**HATUA YA NNE:**

- Hitimisha kwa kuboresha uelewa wa Saratani ya matiti na mpango wa kitaifa wa kuzuia Saratani hii
- Jukumu la watoa huduma ya afya kusaidia huduma ya uchunguzi na tiba ya Saratani ya matiti
- Mwezeshaji atoe muhtasari wa mada,fafanua na fanya majumuisho

**9.4 Kuelimisha wateja kuhusu Saratani ya tezi dume**
**Muda:** Dakika 30
**Njia za uwezeshaji:** Majadiliano na uwasilishaji wa mada kwa kutumia slides
**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki
**Maelekezo kwa mwezeshaji:**
**Hatua ya Kwanza:** Toa muhtasari wa Saratani ya tezi dume Tanzania. Wasilisha kwa kifupi takwimu muhimu kuhusu saratani ya tezi dume kuelimisha washiriki hali halisi nchini
**Hatua ya Pili:** Waelimishe washiriki sababu zinazochangia wanaume kupata Saratani hii na dalili za ugonjwa wa Saratani ya tezi dume
**Hatua ya Tatu:** Waeleze njia mbali mbali za kupunguza uwezekano wa kupata Saratani ya tezi dume na uchunguzi wa Saratani hii
**Hatua ya Nne:** Karibisha maswali na fanya majumuisho

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waulize washiriki swali wabunge bongo kuhusu ukubwa wa tatizo la Saratani ya Tezi dume Tanzania.Hali halisi ikoje kwenye makazi yao?Je wameshawahi kuona mgonjwa mwenye Saratani ya tezi dume ?

- Waeleze washiriki kuwa hapa Tanzania, ugonjwa wa Saratani ya tezi dume umekuwa ukiongezeka kwa miaka kadhaa iliyopita. Kulingana na takwimu za kidunia kutoka report ya Globocan 2012 ilikadiriwa wagonjwa wapya 3434 waligunduliwa na Saratani hii ambao ni takriban asilimia 10 ya wagonjwa woet wa saratani. Saratani ya tezi dume inawaathiri wanaume wengi wenye umri kunzia miaka 60

**HATUA YA PILI:**

- Ongoza majadiliano kuhusu sababu zinazochangia wanaume kupata Saratani ya tezi dume.
- Toa nafasi kwa washiriki kuwasilisha maoni yao
- Angalia slides kuboresha uelewa wao na kufanunua sababu mbalimbali zinavyochangia kusababisha Saratani ya tezi dume
- Waeleze hali halisi nchini Tanzania

**HATUA YA TATU:**

- Tumia slides kuelimisha washiriki kuhusu dalili na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata Saratani ya tezi dume na walengwa kwenye uchunguzi wa Saratani hii
- Karibisha maswali ili kuboreha uelewa wao
- Hakikisha yafuatayo yanatajwa kuhusu dhana inayohusu Saratani ya tezi dume;
    - Sababu zinazochangia wanaume kupata Saratani ya tezi dume
    - Dalili za Saratani ya tezi dume
    - Jinsi ya kuzuia uwezekano wa kupata Saratani ya tezi dume
    - Walengwa wa uchunguzi wa Saratani ya tezi dume
    - Kutambua vituo vinavyoweza kutoa huduma za uchunguzi wa Saratani ya tezi

dume

**HATUA YA NNE:**

- Hitimisha kwa kuboresha uelewa wa Saratani ya tezi dume na mpango wa kitaifa wa kuzuia Saratani hii
- Jukumu la watoa huduma ya afya ya jamii kuhamasisha wanaume kupima saratani ya tezi dume na kutambua dalili za awali
- Toa muhtasari wa mada na fanya majumuisho

**9.5 Majukumu na wajibu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo an Saratani za via vya uzazi**

**Muda:** Dakika 30

**Njia za uwezeshaji:** Majadiliano makundi madogo

**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki/Kiongozi cha mwezeshaji

**Maelekezo kwa mwezeshaji:**

**Hatua ya Kwanza:** Wagawe washiriki kwenye makundi na wajadili kwa dakika 10 majukumu na wajibu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na Saratani za via vya uzazi

**Hatua ya Pili:** Waambie washiriki wawasilishe majibu yao kwa vikundi.Ongeza au sahihisha yaliyojadiliwa

**Hatua ya Tatu:** Fanya majumuisho ya majadiliano

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waambie washiriki wajigawe katika makundi
- Toa nafasi kwa washiriki kujadili majukumu yao katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na Saratani za via vya uzazi

**HATUA YA PILI:**

- Ongoza majadiliano kwa kutoa nafasi ya vikundi kuwasilisha maoni ya kazi zao.
- Boresha uelewa wao na kufanunua wajibu wao kwenye jamii kwa kuangalia mwongozo wa mtoa huduma ya afya kwenye jamii
- Ongeza au sahihisha yaliyojadiliwa

**HATUA YA TATU:**

- Fafanua na fanya majumuisho ya somo
- Boresha uelewa wao kwenye jukumu la watoa huduma ya afya ya jamii kuhamasisha jamii kwenye uchunguzi wa saratani za via vya uzazi

**9.6 Wateja wanaotakiwa kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa saratani ya via vya uzazi**

**Muda:** Dakika 15
**Njia za uwezeshaji:** Mhadhara mfupi
**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki/Kiongozi cha mwezeshaji
**Maelekezo kwa mwezeshaji:**

**Hatua ya Kwanza:** Tumia slide kuelimisha na kutoa nafasi ya washiriki kutambua makundi mbali mbali yanayostahili kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa saratani ya via vya uzazi

**Hatua ya Pili:** Fanya majadiliano, fafanua na majumuisho

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waambie washiriki wataje makundi mbali mbali yanayostahili kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa Saratani za via vya uzazi
- Tumia slides kuboresha uelewa wao
- Toa nafasi kwa washiriki kujadili majukumu yao katika kutekeleza mpango wa rufaa kwa ajili ya saratani ya mlango wa kizazi,matiti na tezi dume

**HATUA YA PILI:**

- Boresha uelewa wao na kufafanunua wajibu wao kwenye jamii kwa kuangalia mwongozo wa mtoa huduma ya afya ngazi ya jamii na tumia slides kuweka msisitizo
- Fafanua na fanya majumuisho

**9.7 Ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi**
**Muda:** Dakika 30
**Njia ya kuwezesha: Igizo dhima**
**Vifaa vya kufundishia:** Chati pindu/ kalamu kubwa ya rangi,gundi ya karatasi

**Maelekezo kwa mwezeshaji:**
**Hatua ya Kwanza:** Toa mada fupi kuhusu ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na saratani za via vya uzazi
**Hatua ya Pili:** Chagua washiriki wa kujitolea kufanya igizo dhima
**Hatua ya Tatu:** Fanya Igizo dhima
**Hatua ya Nne:** Jadili vipengelea vya mchakato wa kutoa ushauri kwa familia/jamii kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi

**HATUA YA KWANZA:**

- Toa mada fupi kuhusu ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na saratani za via vya uzazi
- Toa nafasi kwa washiriki kujadili majukumu yao katika kutekeleza huduma za ushauri

**HATUA YA PILI:**

- Waombe washiriki watano wa kujitolea kufanya igizo dhima
- Mmoja awe mtoa huduma ngazi ya jamii,wa pili awe mgonjwa wa saratani,mmoja awe baba wa familia na mwingine mama wa familia na wa mwisho jirani
- Kisha waelekeze waigize kufuatana na maelekezo ya igizo
- Baada ya kusoma maelekezo ya igizo zima waeleze washiriki wengine kufuatilia ushauri kwa familia jinsi ya kumtunza mgonjwa mwenye Saratani

<table>
<tr><th><u>MUHTASARI WA IGIZO</u></th><th><u>WAHUSIKA KATIKA IGIZO:</u></th></tr>
<tr><td>Mawazo ni mgonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi kwenye ngazi ya nne ya ugonjwa. Anatoa harufu mbaya na anatoka damu ukeni mara kwa mara.hana hamu ya kula ana mawazo mengi na ndugu wamemtenga kwa ajili ya ugonjwa huu na mume amemkimbia. Kwa sasa anaishi na kaka na wifi yake.</td><td>• Mawazo ambaye ni mgonjwa<br>• Bwana na bi Mapinga (kaka na wifi ya mgonjwa)<br>• Jirani_bi Usipitwe<br>• Mtoa huduma ya afya ya jamii Bi Semeni<br><u>ANDIKO:</u><br>• Mwonyeshe mtoa huduma wa afya ngazi ya jamii akionekana anaenda kutoa ushauri nyumbani kwa Mzee Mapinga<br>• Anakuta mgonjwa akiwa kwenye maumivu na masikitiko huku anakula mahindi magumu yaliyochemshwa<br>• Bwana na Bi Mapinga waonyeshe hali ya unyanyapaa na kutomjali mgonjwa kwa vitendo<br>• Jirani aongezee kuchombeza kwa kujifanya mjuaji na kutetea familia ya Mzee Mapinga<br>• Mtoa huduma ya afya awajibike kutoa ushauri kwa mgonjwa na familia kwa nadharia na vitendo kwa kusisitiza:<br>  ○ Umuhimu wa lishe bora<br>  ○ Upendo na uvumilivu kwa familia wakati wa kuuguza<br>  ○ Kuwa karibu na mgonjwa na kumsikiliza mahitaji yake<br>  ○ Kuacha unyanyapaa</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| | ○ Kumpeleka kituo cha afya pale inapobidi<br>○ Kuelimisha kuhusu ugonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi na dalili za ugonjwa huu |

**HATUA YA TATU:**

- Jadili vipengele mbali mbali ikiwepo maana ya igizo hili na mafundisho yaliyomo ndani ya igizo
- Hitimisha kwa kuweka msisitizo juu ya wajibu wa mtoa huduma ya afya kwenye jamii na majirani kusaidia wagonjwa wa Saratani ya via vya uzazi
- Tumia slides kuboresha uelewa wao

## 9.8 Kuanisha imani na fikra potofu ndani ya jamii kuhusu Saratani ya via vya uzazi

**Muda:** Dakika 15
**Njia za uwezeshaji:** Mhadhara mfupi
**Vifaa vya kuwezesha:** Chati pindu/ Projekta ya elektroniki/Kiongozi cha mwezeshaji
**Maelekezo kwa mwezeshaji:**

**Hatua ya Kwanza:** Tumia slide kuelimisha na kutoa nafasi ya washiriki kutambua na kujadili imani na mila potofu ndani ya jamii kuhusu saratani ya via vya uzazi

**Hatua ya Pili:** Fanya majadiliano, fafanua na majumuisho

.

**HATUA YA KWANZA:**

- Waambie washiriki wataje mila potofu wanazozisikia na wanazozifahamu kutoka kwenye jamii zao kuhusu saratani
- Tumia slides kuelimisha na kuboresha uelewa wao
- Toa nafasi kwa washiriki kujadili majukumu yao katika kuelimisha jamii kwenye mila na imani potofu zinazohusu Saratani za via vya uzazi

**HATUA YA PILI:**

- Boresha uelewa wao, eleza ukweli kuhusu elimu inayohusu saratani husika na wajibu wao kwenye jamii.
- Fafanua na fanya majumuisho

**FOMU YA RUFAA**

**Jina la mteja ……………………………………………………………………………**
**Jina la Mhudumu wa Afya katika jamii……………………………….…………**
**Anuani (Kijiji/Kata/Wilaya)……………………………………….……………….**
**Rufaa Kwenda (Jina la Kituo cha huduma) ……………………………………**

| **Tatizo/Hali** | **WekaVema(ü)** |
|---|---|
| **HUDUMA ZA SARATANI YA VIA VYA UZAZI** | |
| **Tatizo/Hali** | |
| Kufanya uchunguzi wa Saratani ya via vya uzazi: | |
| Mlango wa kizazi | |
| Dalili za Saratani ya via vya uzazi; | |
| Mlango wa kizazi | |
| Matiti | |
| Tezi dume | |

Huduma aliyopewa kabla ya rufaa……………....…………………………………………

**Sahihi………………………Tarehe……………………………Muda………………………**

**Kata hapa**

**…………………………………………..……………………………………………………**

**FOMU YA MREJESHO BAADA YA RUFAA**

Jina la mteja/mgonjwa…………………………………………………………………………

Utambuzi wa ugonjwa…………………..…………………………………………………...

Huduma aliyopewa……………………………………………………………………………..

Maoni……………………………………………………………………

Ufuatiliaji(Tarehe)…………………………………………………………

Jina la Mhudumu wa Afya…………………………………

Sahihi……………..Tarehe………………………

**FOMU YA MUHTASARI WA ROBO MWAKA YA HUDUMA JUMUISHI ZA AFYA YA U Z A Z I , MAMA, MTOTO MCHANGA, MTOTO UMRI CHINI YA MIAKA MITANO NA VIJANA KATIKA JAMII**

Mkoa: ……………………………………….. Wilaya: .....................................................................
Jina za Vituo vya Kutolea Huduma za Afya: ........................................................................................
Taarifa ya Miezi/Mwaka: ……………..…… Tarehe ya kuwasilisha Taarifa: ...........................................

| Jumla ya rufaa zilizotolewa | |
| --- | --- |
| **Saratani ya Via vya Uzazi** | |
| Idadi ya wanawake waliopewa rufaa kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kupata uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi | |
| Idadi ya wanawake waliopewa rufaa kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kupata uchunguzi wa saratani ya matiti | |
| Idadi ya wanaume waliopewa rufaa kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kupata uchunguzi wa saratani ya tezi dume | |